# DARASA LA SABA

# KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda:Saa 1 dakika 40**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

Ulikuwa usiku ___ 1 ___ manane. Mvua ___ 2 ___ kwa kiasi kikubwa. Nje kulikuwa na giza ___ 3 ___. Kijiji ___ 4 ___ kilikuwa kimelala. ___ 5 ___ ya vyura vidimbwini ndiyo iliyosikika. Ghafla bin vuu ___ 6 ___ yalienea angani kutoka ___ 7 ___ nyumba ya jirani. Mbwa nao walisikika ___ 8 ___. Wanakijiji walitetemeka kwa ___ 9 ___ walihofia maisha yao. Hakuna aliyeelewa ___ 10 ___ za usiahi huo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** A. ya | B. kwa | C. na | D. wa |
| **2.** A. ilinyesha | B. zilinyesha | C. ulinyesha | D. walinyesha |
| **3.** A. tititi | B. mwa | C. totoro | D. tiriri |
| **4.** A. mzima | B. kizima | C. nzima | D. zima |
| **5.** A. Milio | B. Mroromo | C. Kulia | D. Mlio |
| **6.** A. sauti | B. nduru | C. ugomvi | D. mayowe |
| **7.** A. kwa | B. katika | C. ndani | D. juu ya |
| **8.** A. wakilia | B. wakikoroma | C. wakibweka | D. wakiwika |
| **9.** A. woga | B. furaha | C. raha | D. kicheko |
| **10.** A. ukweli | B. faida | C. hasara | D. sababu |

Ni ___ 11 ___ la kuvunja moyo kuona jinsi nchi yetu inavyodidimia katika ufisadi. Pesa ___ 12 ___ zimefujwa na viongozi wetu wenye ___ 13 ___ ya fisi. Wao huendelea tu kujaza matumbo ___ 14 ___. Tushirikiane kupigana na ufisadi kwani ___ 15 ___.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **11.** A. shughuli | B. jambo | C. nia | D. mambo |
| **12.** A. mingi | B. mengi | C. nyingi | D. wengi |
| **13.** A. tamaa | B. matumaini | C. uroho | D. hamu |
| **14.** A. zao | B. yake | C. yenu | D. yao |

**15.** A. asiyesikia la mkuu huvunjika guu B. mvumilivu hula mbivu
C. umoja ni nguvu utengano ni udhaifu D. dalili ya mvua ni mawingu

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Ni salamu zipi zinazotumiwa na watoto?

A. Chewa - chewa

B. Hujambo - sijambo

C. Cheichei - ewaa

D. Shikamoo - marahaba

**17.** Andika sentensi ifuatayo kwa wingi

Uzi huo ndio ulioshonea nguo

A. Nyuzi hiyo ndiyo iliyoshonea nguo

B. Uzi hizo ndizo zilizoshonea nguo

C. Nyuzi hayo ndiyo yaliyoshonea nguo

D. Nyuzi hizo ndizo zilizoshonea nguo

**18.** Ni kiungo kipi cha mwili kinachosafisha damu?

A. Figo

B. Ini

C. Kongosho

D. Kibofu

**19.** Akisami $^2/_9$ kwa maneno ni ______

A. sudusi tisa

B. tusui mbili

C. subui tisa

D. thumni mbili

**20.** Ni sentensi ipi iliyo katika hali timilifu?

A. Wageni walifika asubuhi

B. Miti hiyo itakatwa kwa shoka

C. Mwalimu anafunza Kiswahili

D. Wanafunzi wamefika shuleni

**21.** Kutokana na nomino <u>ulezi</u> tutapata kitenzi kipi?

A. Malezi

B. Lea

C. Mzazi

D. Mlinzi

**22.** Shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti huitwa?

A. Takhmisa

B. Tarbia

C. Tasdisa

D. Tathnia

**23.** Ipi si maana ya neno vua?

A. Ondoa mwilini kitu kilichovaliwa

B. Toa samaki majini

C. Toa mtu katika matatizo

D. Safisha nguo kwa maji na sabuni

**24.** Kanusha sentensi ifuatayo kwa usahihi

Kusoma sana kulimsaidia baadaye.

A. Kusoma sana hakukumsaidia baadaye

B. Kutosoma sana hakutamsaidia baadaye

C. Kutosoma sana hakukumsaidia baadaye

D. Kusoma sana hakutamsaidia baadaye

**25.** Chagua sentensi yenye istiara

A. Mwanafunzi ni kigeugeu kama kinyonga

B. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

C. Gunia lilianguka sakafuni pu

D. Mtu huyu ni sungura

26. Maneno dhana na zana, nchi na inchi, dhalili na dalili huitwa?

A. Visawe
B. Vitate
C. Vitawe
D. Vibadala

27. Tegua kitendawili kifuatacho.
Chaudhi, chapendeza, chachekesha

A. Sauti
B. Upara
C. Hewa
D. Ndege

28. Ni alama ipi ya uakifishaji inayoonyesha kuwa kuna orodha itakayofuata?

A. Nukta na mkato
B. Mabano
C. Nukta mbili
D. Kikomo

29. Chagua mkato wa mpwa wako.

A. Mpwawo
B. Mpwako
C. Mpwawe
D. Mpwao

30. Ni methali ipi yenye maana kuwa vitendo vyema kila wakati hupongezwa na mtu husifiwa kwa matendo yake mema?

A. Chanda chema huvikwa pete
B. Yaliyopita si ndwele tugange yajayo
C. Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji
D. Usipoziba ufa utajenga ukuta

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Hivi majuzi, yaani siku ya Dominika iliyopita, nilikata shauri kuliabiri basi ili kwenda kumzuru na kumjulia hali shangazi yangu ambaye sikuwa nimemtia ozi kwa muda mrefu. Shangazi yangu alikuwa akiishi mtaa wa vumilia umbali wa kilomita hamsini hivi upande wa mashariki mwa jiji nilimoishi.

Naam, basi lilikuwa limejaa abiria ungedhani ni ndizimkunguni. Kila mmoja alikuwa katika shughuli zake. Pengine kuna wale waliokuwa wakitoka kazini kurejea kwao kuburudika baada ya siku nzima ya kuraukia kazi. Wengine huenda walikuwa wakitoka maabadini. Ndani mlikuwa na joto kama tanuri lakini nilivumilia bora tu nifike mapema.

Barabara hiyo haikuwa na magari mengi ya abiria. Punde si punde dereva alilitia gari ufunguo na safari ikaanza mwendo wa saa tisa unusu. Safari sasa ilikuwa imeiva. Abiria walisikika wakipiga gumzo na wengine wakiangua vicheko. Hiyo ilikuwa ishara ya furaha.

Baadaye kondakta alisimama na kuanza kazi yake ya kuchukua nauli huku akipeana risiti. Alipofika nilipokuwa nimeketi, alininyooshea mkono akidai nimpe haki yake. Bila ya wasiwasi wala wahaka wowote niliupeleka mkono mfukoni ili kutoa pesa za nauli.

Masalaale!Moyo ulianza kunienda mbio nilipokosa hela mfukoni. Acha kijasho chembamba kinidondoke kipajini. Nilijaribu kuongea lakini sauti haikunitoka. Kumbe huenda nilizipoteza pesa zangu pale stendini. Abiria mmoja alinionea huruma na kunilipia nauli ya shilingi mia mbili kwani kondakta alikuwa ametishia kunitupa nje. Nilimshukuru abiria huyo kwa wema wake. Baada ya saa mbili, nilifika kwa shangazi salama salimini.

**31.** Msimulizi alienda kumtembelea shangazi yake siku gani?
A. Jumatatu
B. Jumapili
C. Jumamosi
D. Ijumaa

**32.** Ni nini maana ya maneno <u>nimemtia ozi</u> kulingana na habari?
A. Nimemsikia
B. Nimemtembelea
C. Nimemwona
D. Nimemkuta

**33.** Kulingana na habari hii, ni kweli kusema;
A. msimulizi aliishi katika mji wa Vumilia
B. mtaa wa Vumilia ulikuwa magharibi mwa alipoishi msimulizi
C. mtaa wa Vumilia ulikuwa umbali wa kilomita mia moja
D. shangazi ya mwandishi aliishi katika mtaa wa Vumilia

**34.** Basi alilolisafiria msimulizi;
A. lilikuwa na abiria wengi zaidi
B. liliendeshwa kwa kasi
C. halikuwa na abiria wengi sana
D. lilibeba abiria kiasi tu

**35.** Katika basi hilo si kweli kusema kuwa;
A. kila abiria alitoka shughuli zake
B. abiria wote walikuwa wakitoka kazini
C. miongoni mwa abiria kuna wale waliotoka maabadini
D. basi lilikuwa na joto jingi

**36.** ......<u>joto kama tanuri</u>. Hii ni fani gani ya lugha?
A. Istiara
B. Methali
C. Tashbihi
D. Nahau

**37.** Ni jambo lipi linaloonyesha kuwa abiria walikuwa wenye furaha?
A. Kucheza kutokana na muziki uliokuwa basini
B. Kupiga gumzo na kucheka
C. Kucheka na kupeana nauli
D. Kuzungumza na kuwa na wasiwasi

**38.** Pindi tu kondakta alipomnyooshea mkono msimulizi ampe nauli
A. Alijitia hamnazo ili kuepuka kulipa nauli
B. Tayari alikuwa amefahamu alipoteza pesa zake
C. Alianza kulia kwani hakuwa na pesa za kulipia nauli
D. Aliupeleka mkono mfukoni ili kutoa pesa za nauli

**39.** Baada ya msimulizi kugundua kuwa hakuwa na hela mambo yafuatayo yalitokea isipokuwa?
A. Alipata ujasiri mkubwa
B. Moyo ulimdunda kwa kasi
C. Jasho lilimtiririka usoni
D. Alishindwa kuzungumza

**40.** Abiria aliyemlipia msimulizi nauli alikuwa mwenye
A. kichwa chepesi
B. mkono wazi
C. kulaza damu
D. mkono birika

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50.</u>***

Ulanguzi na utumiaji wa dawa za kulevya ni jambo lililopigwa marufuku na kupigwa vita na mataifa mengi ya dunia. Serikali za nchi duniani zimekuwa macho <u>kuwatia mbaroni</u> wanaohusika na ulanguzi huu.

Katika jitihada hizi wanaotoka na wanaoingia nchini huchunguzwa ili kuonekana kama wanasafirisha dawa za kulevya. Utafiti unaonyesha kuwa watu wengi wanaopatikana na hatia hii huadhibiwa vikali.

Dawa za kulevya zina madhara ambayo kila aliye na sikio angezingatia mafunzo dhidi yake. Kwa kufanya hivyo watajitahidi kujiepusha nazo au kuziacha ikiwa wanahusika nazo. Dawa hizi zimewafanya wengi kuwa mazuzu baada ya kuzitumia kwa muda mrefu kupita kiasi hata zikawadhuru akili zao.

Watoto wa watu, wanaotumia mihadarati huzaliwa wakiwa na kasoro fulani katika viungo vya miili yao. Aidha, huwa na uzani mdogo. Wengine huadhirika akilini na kusababisha shida za kutofanya uamuzi mwafaka akilini na pia kuwa na matokeo mabaya shuleni.

Wakati mwingine dawa hizi humfanya mtumiaji asione vizuri. Macho huona vitu vidogo vikiwa vikubwa na vikubwa vikiwa vidogo. Kutoona vyema huku huwafanya madereva wanaotumia dawa hizi kusababisha ajali barabarani.

<u>Maji yanapozidi unga,</u> watumiaji wa dawa hizi huipa dunia mkono wa buriani. Ni jukumu letu kushikana mikono na kupinga ulanguzi wa dawa za kulevya tusije tukaangamia sote.

41. Ulanguzi na utumiaji wa dawa za kulevya unapingwa katika
A. mataifa yote duniani
B. serikali zote duniani
C. mataifa mengi Afrika
D. Nchi nyingi duniani

42. Ni nini maana ya <u>kuwatia mbaroni</u> kulingana na habari?
A. Kuwafukuza
B. Kuwakamata
C. Kuwazuia
D. Kuwatenga

43. Wanaopatikana na hatia hufanyiwa nini?
A. Huadhibiwa vikali
B. Husamehewa na kuachiliwa
C. Hurudishwa katika nchi walizotoka
D. Hutengwa wasiwadhuru wengine

44. Yafuatayo ni madhara ya mihadarati isipokuwa;
A. kasoro kwenye akili
B. matatizo ya macho
C. watoto kuzaliwa wakiwa na uzani mdogo
D. kuchangamsha akili na kuwa zuzu

45. Ni nini kinachosababisha ajali kulingana na habari?
A. Madereva kukosa usingizi wa kutosha
B. Madereva kutoona vizuri
C. Madereva kuwa na fikra nyingi
D. Madereva kubeba abiria wengi

46. Ni kweli kusema kuwa
A. dawa hizi zinapotumiwa kwa muda mrefu haziathiri akili
B. watoto wa wanaotumia mihadarati huugua utapiamlo
C. watoto wanaozaliwa na wanaotumia mihadarati hawafaulu masomoni
D. dawa za kulevya hazina madhara mengi

47. Unafikiria ni orodha gani yenye dawa za kulevya pekee?
A. Pombe, sigara, kahawa
B. Miraa, kokeini, mchicha
C. Miraa, dania, pombe
D. Pombe, sigara, miraa

48. Ni nini maana ya <u>maji yanapozidi unga</u> kulingana na habari?
A. Mambo yanapokuwa mabaya
B. Mambo yanapokuwa mengi
C. Mambo yanapokosa kufaulu
D. Mambo yanapoonekana kuboreka

49. Ni wajibu wetu kufanya nini?
A. Kutengana ili tusiathirike na dawa za kulevya
B. Kuungana pamoja kuwaangamiza watumiaji wa mihadarati
C. Kushirikiana na kupigana na mihadarati
D. Kushirikiana na kupigana na mihadarati

50. Kichwa kinachofaa habari hii ni kipi?
A. Madhara ya dawa za kulevya
B. Aina za dawa za kulevya
C. Matumizi ya dawa za kulevya
D. Njia za kuzuia dawa za kulevya